**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA**

*Barua zote zitumwe kwa:*

**Simu:** +255 28 2224013

**Faksi:** +255 28 2224168

**Mkurugenzi Mtend**
**S. L.**
**Muleba,**

*Unapojibu tafadhali taja*

**BaruaPepe:**ded@mulebad

**Kumb Na. KGR/MLB/HW/ A.12/VOL.I /31**

**Tarehe** 17/08

# *TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MUDA*

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Muleba anapenda kuwatangazia wananchi wote nafasi za kazi ya ajira ya muda kwa madereva 6, Mtangazaji Msaidizi 2, Mwandishi wa habari wa redio 1 na wakusanya ushuru 30.

1. **JINA LA KAZI DEREVA II (NAFASI 6)**

**A. MAJUKUMU**

i. Kukagua gari kabla ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali za Serikali,
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (log book),
vi. Kufanya usafi wa gari na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

**B. SIFA YA MWOMBAJI**

i. Awe na Elimu ya kidato cha nne na kuendelea
ii. Awe na leseni Daraja E au C1 au C ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.
iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
iv. Mwombaji asiwe na umri unaozidi miaka arobaini na tano (45)
v. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiliwa kwanza.
vi. Awe mwadilifu
vii. Awe Mtanzania
viii. Awe na Kitambulisho cha Taifa (NIDA)

**C. NGAZI YA MSHAHARA TGS B**

2. **MTANGAZAJI MSAIDIZI (NAFASI 2 )**

**A. MAJUKUMU**

i. Kusaidia watangazaji kuandaa "scripts" za muziki na matangazo
ii. Kusaidia kutangaza na kurekodi ndani na nje ya studio
iii. Kusaidia utafiti wa vipindi vya redio, usikivu na biashara

**B. SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe na Elimu ya kidato cha nne au sita na ufaulu wa masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Sanaa
ii. Awe na cheti cha fani ya Uhandishi wa habari toka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
iii. Awe amehudhulia mafunzo ya muda wa mwaka mmoja wa kazi ya utangazaji au fani ya uandishi wa habari katika chuo kinachotambuliwa na Serikali na kufaulu mtihani wa kupima kipaji.
iv. Awe mwadilifu
v. Awe Mtanzania
vi. Awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA)

**C. NGAZI YA MSHAHARA TGS B**

3. **MWANDISHI WA HABARI WA REDIO (NAFASI 1)**

**A. MAJUKUMU**

i. Kukusanya habari za matukio mbalimbali
ii. Kurekodi taarifa za habari za redio za nchi mbalimbali ulimwenguni
iii. Kufanya kazi chini ya mwandishi wa habari mzoefu

**B. SIFA ZA MWOMBAJI**

iv. Awe na Elimu ya kidato cha nne au sita na ufaulu wa masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Sanaa
v. Awe na cheti cha fani ya Uhandishi wa habari toka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
vii. Awe amehudhulia mafunzo ya muda wa mwaka mmoja wa kazi ya utangazaji au fani ya uandishi wa habari katika chuo kinachotambuliwa na Serikali na kufaulu mtihani wa kupima kipaji.
viii. Awe mwadilifu
ix. Awe Mtanzania
x. Awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA)

**C. NGAZI YA MSHAHARA TGS B**

4. **WAKUSANYA USHURU (NAFASI 30)**

**A. SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea ambao wana uelewa wa kutumia simu ya tachi, sababu Mapato yote ya serikali yanakusanywa kwa kutumia mashine za kielectronic za kukusanyia Mapato (POS) ambayo ina matumizi sawa na simu za tachi.

ii. Awe amefaulu masomo ya Hisabati, Utunzaji wa Vitabu (Book Keeping), Kiswahili na Kiingereza pamoja na mafunzo ya ukusanyaji mapato.

iii. Awe na Afya nzuri

iv. Awe mwadilifu

v. Awe Mtanzania

vi. Awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA)

vii. Awe na umri kuanzia 18 - 40

**B. MAJUKUMU YA KAZI**

i. Kukusanya Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia mashine za kielectronic za kukusanyia Mapato (POS)

ii. Kuhakikisha Fedha inayokusanywa inapelekwa bank kwa wakati

iii. Kuhakikisha Mapato yote yanayopaswa kukusanywa na Halmashauri yanakusanywa kwa usahihi.

**MSHAHARA KWA MWEZI NI TSH.180,000.00/=**

**D. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI YA NAFASI ZA KAZI**

i. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono

ii. Barua za maombi ya nafasi za kazi ziandikwe kwa:

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA,**
**S.L.P 131,**
**MULEBA.**

**iii. MWOMBAJI AAMBATANISHE**

- Curriculum Vitae (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika
- Nakala za vyeti vya Elimu ya Sekondari na Chuo
- Hati ya kuzaliwa (Birth Certificate)
- Picha moja ya PASSPORT SIZE" ya hivi karibuni
- Nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)

**iv. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- Barua za uthibitisho/matokeo ya mitihani (Testimonals/ provisional/ statements of result hazitapokelewa

- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa kama mamlaka husika (TCU na NECTA)
- Waombaji waliostafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- Uwasilishaji wa taaarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

**TANGAZO HILI LA NAFASI YA KAZI YA MUDA LINAFUTA TANGAZO LENYE KUMB.NA.KGR/MLB/HW/A.225/VOL.III YA TAREHE 17/08/2021.**

**MWISHO WA KUPOKEA BARUA ZA MAOMBI HAYO NI TAREHE 01/09/2021 SAA 04:00 ASUBUHI.**

***WOTE WENYE SIFA WANAKARIBISHWA***

Stewart K. Mtondwa,
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**MULEBA.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W) MULEBA